

Ndugu waheshimiwa, wapendwa wanafunzi na marafiki zetu,

ni furaha yetu kubwa kuwatangazia kikao kifuatacho cha

**Baraza letu la Kiswahili la Berlin (BALAKI-BE) la tarehe 13 Januari 2025**

**Fasihi Tafsiriwa kwa Kiswahili: Mtazamo wa Kihistoria kuhusu Dhima na Mchango wake**

**Serena Talento**

Katika wasilisho hili, Serena Talento atachunguza dhima za tafsiri za fasihi ya kigeni kwa Kiswahili katika vipindi vitatu: tendi za kabla ya ukoloni, fasihi zilizotafsiriwa chini ya Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki, na tafsiri za wakati wa enzi za ujamaa. Vilevile, atazungumzia maendeleo ya kisasa katika usambazaji wa fasihi ya kigeni. Kwa mtazamo wa kihistoria na kisosiolojia, atalenga kuonyesha kwamba dhamira ya tafsiri hajishughulishi tu na fasihi bali inahusiana pia na masuala ya kiutamaduni, kiitikadi na kisiasa. Wasilisho lake litakusudia kutambulisha umuhimu wa kusoma tafsiri ya fasihi ili kuelewa historia na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili na mchango wake katika mijadala ya kimataifa ya masomo ya tafsiri.

**Serena Talento** ni Profesa Msaidizi katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, ambapo anafundisha Kiswahili na masomo ya tafsiri katika muktadha wa Kiafrika. Pia ni Mtafiti Mshirika katika Chuo Kikuu cha Free State na Kituo cha Tsikinya-Chaka, Chuo Kikuu cha Witwatersrand. Yeye ni mmojawapo wa wahariri wa jarida la mtandaoni la *Swahili Forum*.

Kikao kitafanyika **siku ya Jumatatu, tarehe 13 Januari 2025, saa kumi za Ulaya ya Kati** (saa kumi na mbili za Afrika Mashariki) **kupitia njia ya Zoom:**  
<https://us02web.zoom.us/j/85426612953?pwd=JT2QQMu3YQ4mG46PHY6xjvPsUdJNZ7.1>

**KARIBUNI NYOTE!**

Tafadhalini wajulisheni wapenzi wote wa Kiswahili na marafiki wengine!

Wasalaam,

Kai Kresse, Lutz Diegner na Maxwell Omondi Ondieki

*Kama kuna maswali yoyote kuhusu baraza hili tafadhalini mwandikieni mwenzetu:*  
<MaxwellOmondi.Ondieki@zmo.de >